**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI BALANG'DALALU**
**S.L.P. 67, KATESH.**

Kumb. Na BSS/JON/…….

JINA LA MWANAFUNZI……………………………………….. S.L.P……………………….
…………………………….

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2024.

**1.0. Utangulizi.**

Ninayofuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Balang'dalalu kwa Muhula wa masomo unaoanza January,2024. HONGERA SANA!

Shule ya Sekondari Balang'dalalu ipo Mkoa wa Manyara Wilaya ya Hanang'. Shule hii ni ya wasichana na wavulana- mchepuo wa kilimo, kwa kidato cha Kwanza hadi cha Nne, na Mchepuo Sanaa kwa Kidato cha Tano hadi Kidato cha Sita kwa Wavulana tu.

Shule ipo umbali wa kilometa 22 kusini mwa mji wa Katesh- ambao ni makao makuu ya Wilaya ya Hanang'.

Magari ya kufika shuleni yanapatikana katika stendi ya magari ya mji mdogo wa Katesh. Huduma ya usafiri ipo kuanzia saa 4.00 asubuhi hadi saa 10 jioni. Nauli ni Tsh.2,500/=.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 08 January, 2024. Wanafunzi wanatakiwa kuripoti shuleni kwa wakati. Wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza January 2024, waripoti ndani ya siku 14 tangu shule kufunguliwa. Wanafunzi Watakao chelewa baada ya siku 14 tangu shule kufunguliwa **HAWATOPOKELEWA!**

## 2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2:1. Sare za shule

Shule ya Sekondari Balang'dalalu inatumia sare za aina mbili, ambazo ni sare ya darasani na sare ya kazi za nje (shamba dress).

**Wavulana**: Suruali 2 za rangi ya **"light bluu"** isiyo fubaa, kitambaa kinapatikana Shuleni pia kwa atakaye hitaji. Mashati 02 **"light blue"**(mikono mifupi), Masweta 2 rangi **" light bluu''**.Tshirt 2 rangi ya kijivu yenye kola. (hii ni sare ya darasani). Tai 2 ndefu rangi ya bluu bahari yenye mistari myeupe. Track suit 1 yenye rangi Kijivu. Viatu vyeusi vya kamba jozi 2. Soksi rangi ya khaki au nyeusi jozi 2.

**Wasichana: . Sketi 2 za rangi ya "light bluu" kitambaa kinapatikana shuleni** pia.

Mashati 2 rangi ya **"light bluu"** (mikono mifupi), Masweta 2 **"light bluu''** . Tshirt 2 rangi ya kijivu ( hii ni sare ya darasani)

Tai 02 ndefu rangi ya bluu bahari yenye mistari myeupe . Track suit 1 rangi ya kijivu, Viatu vyeusi vya kamba jozi 2, .Soksi nyeupe(ndefu) jozi 2

**2:1. SARE ZA NJE (Shamba dress):**

**Wavulana: .** Suruali 2 rangi ya khaki, ishonwe yenye marinda mawili,kulia na kushoto (celebration) upana chini isipungue nchi 14, urefu ifike kwenye viatu, ashonewe aje nayo akiwa ameivaa wakati unaripoti (mshonee suruali mbili za khaki). Tshirt 2 rangi nyeusi yenye kola isiwe na maandishi yoyote,,nunua mbili. ivaliwe na suruali ya Khaki wakati unaripoti shuleni January 2024.

**Wasichana:** Sketi 2 rangi ya khaki ishonwe mshono wa rinda box,mbili, rinda moja nyuma na rinda la pili mbele,sketi iwe na urefu wa nchi 8 chini ya magoti, njoo nayo moja ukiwa umeivaa. Tshirt 2 rangi nyeusi yenye kola isiwe na maandishi yoyote. Sketi ya Khaki ivaliwe na Tshirt nyeusi wakati mwanafunzi anapo ripoti shuleni January 2024

**USHONAJI WA SARE YA DARASANI PAMOJA NA VIPIMO**

- **Suruali ishonwe ndefu inayofika kwenye viatu, upana chini isipungue nchi 14, iwe na rinda mbili kulia na rinda mbili kusho, nyuma iwe na mfuko mmoja.**
- **Sketi ishonwe ndefu hesabu nchi 8 kutoka kwenye magoti, iwe na rinda box moja mbele na rinda box moja nyuma.**

**KUMBUKA:**

**** VITAMBAA, MASHATI, MASWETA, TSHIRT, TRACK SUITS NA TAI**

**VINAPATIKANA SHULENI KWA BEI RAFIKI KWA MZAZI ATAKAYE HITAJI HUDUMA HIYO ****

**KWA MZAZI ATAKAYE HITAJI HUDUMA YA SARE PIGA SIMU HIZI KWA AJILI YA MAELEKEZO**

**SIMU 0783868000 NA 0754775502**

**2.3) SARE ZA MICHEZO**

- . **Wavulana**: Bukta 2 nyeusi, nunua na njoo nazo shuleni.
- **Wasichana**: Bukta 2 nyeusi, nunua na njoo nazo shuleni
- Raba za michezo rangi yoyote, mnunulie mwanafunzi

**3.0 MAHITAJI YA TAALUMA**

- Kalamu 10
- Penseli za kutosha
- .Daftari (counter book Quire 2) – 10
- Mkebe wa hisabati mpya 01
- Begi la kubebea madaftari

**4.0 –MAHITAJI YA VIFAA VYA MALAZI (nunua na uje navyo shuleni)**

- Godoro moja futi mbili na nusu,unene usipungue inch 3.
- Chandarua 1 – iliyowekwa dawa, Blanketi1,Mashuka mawili (2), rangi bluu kwa wavulana na kwa wasichana rangi ya Pink mto 1 na foronya.

**4:1: VYOMBO VYA CHAKULA ( nunua uje navyo)**

- Bakuli 1 Sahani 1,.Kikombe 1, Kijiko 1**,**

****(vyombo vyote viwe vya bati)** vyombo vya plastiki haviruhusiwi kuingizwa shuleni.**

**5:0 MAHITAJI MENGINE**

**5:1. Huduma ya Afya na matibabu**.

Kila mzazi ahakikishe anamkatia mwanae **BIMA** ya Afya atakayo itumia kugharamia matibabu. Aidha kwa wale watakao shindwa kupata BIMA ya AFYA, waje na Fedha taslimu TSH.50400/= kwa ajili ya kulipia BIMA YA AFYA YA TAIFA ( NHIF)

**NB**: Shule inatoa huduma ya kwanza tu.

**5:2 MAHITAJI MENGINE YA MUHIMU AMBAYO MZAZI ANATAKIWA KUNUNUA**

- Ndoo 2, moja kubwa na moja ndogo.,Fagio 1 aina ya chelewa , Jembe 1 lenye mpini, ufagio wa kudekia 1( mopper) au ufagio brash wa kufanyia usafi bwenini, mabafuni na vyooni.
- **SANDUKU MOJA IMARA LA CHUMA, LIWE KUBWA LENYE KUFUNGWA NA VITASA VIWILI.**

## 6:0 SHERIA ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI zenye dhamana na jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu Nchini.

****Sheria zingine ndogo ndogo za shule utapewa na kusomewa ufikapo shuleni****

## 7:0 MAMBO MENGINE YA KUZINGATIWA.

7:1 Jaza na kuleta medical examination form – kiambatisho B.

- Formu hii itajazwa na mganga katika hospitali ya serikali.

7: 2. Fomu ya mzazi kukiri kukubali mwanae kusoma katika shule hii.

- Pia mwanafunzi kukubali kusoma katika shule hii na kufuata sheria za shule (kiambatisho A.)

**KARIBU SANA BALANG'DALALU SEKONDARI**

…………………………

**Yuda A. Fissoo**

**MKUU WA SHULE MAWASILIANO:**

1. **0759 795 098 MKUU WA SHULE**
2. **0755 900 058 MAKAMU MKUU WA SHULE**

# PRESIDENT'S OFFICE
# REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

**BALANG'DALALU SECONDARY SCHOOL**

**KIAMBATANISHO "B"**

MEDICAL EXAMINATION FORM

Government medical Officer,

…………………………………..
…………………………………..
…………………………………..
………………………………….

Please examine…………………………………………………………………….
(Name of a student) Who has been selected to join school for his/her fitness as student moray in the following:-

1. Vision……………………………………………………
2. Hearing………………………………………………….
3. Urine…………………………………………………….
4. Stool……………………………………………………..
5. Blood……………………………………………………
6. Asthma……………………………………………………
7. Tuberculosis
8. Pregnancy (female)……………………………………….. 9. Any other findings and comments:………………………..
   ……………………………………………………………
   …………………………………………………………….
   ……………………………………………………………

**<u>MEDICAL CERTIFICATE</u>**
(to be completed by the government medical officer)
I have examined the student named above and recommend that he/she is physically Fit/unfit as a student

Date:………………… Signature……………………..
Station ………………... Designation………………….

**NB: Please return this form to school in sealed envelope**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA SHULE YA SEKONDARI BALANG'DALALU**

**KIAMBATANISHO "A FOMU**

**YAH: KUKUBALI SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE**

**( MWANAFUNZI AJAZE SEHEMU HII )**

1. Mimi ……………………………………………….msichana/mvulana ninakubali kuingia kidato cha kwanza shule ya Sekondari Balan g'dalalu.
   Tarehe………………….na nitafika shuleni bila kuchelewa.
   Nitatii sheria za shule na nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kwenye kazi za nje. Mungu nisaidie.
2. Anwani yangu ya kudumu ni

____________________________

3.Sahihi ya mwanafunzi____________________

**MZAZI/MLEZI AJAZE SEHEMU HII**

Mimi …………………………………………………nakubali

Mtoto wangu…………………………………………(jina) asome katika shule ya sekondari Balang'dalalu. Naahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyooneshwa katika barua ya masharti ya kujiunga na shule hii.

Naahidi kuwa nitamsihi kutii sheria zote za shule na kuwa na bidii kwenye masomo na kwenye kazi za nje pia.

Anwani yangu ya kudumu ni

____________________________

____________________________

____________________________

Sahihi ………………………………………………………tarehe ……………..

**Wageni ninaowaidhinisha kuja kumwona mwanangu awapo shuleni muda maalumu ulio pangwa na shule ni kila Jumamosi na Jumapili za mwisho wa miezi tu.(Wasizidi wawili)**

JINA UHUSIANO